https://dspace.org/

# Ushairi Wa Kezilahabi Ni Ushairi Wa Nabhany: Ushahidi Kutoka Uchanganuzi Wa Umbo La Shairi La Wanajadi

**Karama, Mohamed; Mwamzandi, Issa**

**2019-04-10**
Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/421
Karama, M., & Mwamzandi, I. (2019). Ushairi wa Kezilahabi ni Ushairi wa Nabhany: Ushahidi Kutoka Uchanganuzi wa Umbo la Shairi la Wanajadi. Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili, 1(1), 7-12.

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 4, Issue 1, 2019
ISSN: 1476-4687

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# USHAIRI WA KEZILAHABI NI USHAIRI WA NABHANY: USHAHIDI KUTOKA UCHANGANUZI WA UMBO LA SHAIRI LA WANAJADI

*Mohamed Karama[1] & Issa Mwamzandi[2]*,

[1]Chuo Kikuu cha Kabianga, S.L.P 2030-20200, Kericho, Kenya, mkarama@kabianga.ac.ke
[2]Chuo Kikuu cha Kabianga, S.L.P 2030-20200, Kericho, Kenya, imwamzandi@kabianga.ac.ke

**Article history:**

*Received: 20 Mar 2019*
*Accepted: 02 Apr 2019*
*Published: 10 Apr 2019*

**Keywords**:

*Ushairi*
*Kezilahabi*
*Nabhany*
*Uchanganuzi*
*Wanajadi.*

## MUKHTASARI

Makala haya yanakariri hoja kwamba ushairi wa Wagunduzi ni ushairi wa Wanajadi. Mapitiyo yetu ya maandishi yanayozungumziya ushairi wa Kiswahili yameonesha kwamba kuna makundi mawili: Wanajadi, akiwamo Sheikh Nabhany, na Wagunduzi, akiwamo Kezilahabi. Yaliyoandikwa yanaonesha kuwa mgogoro ulizuka kutokana na wanajadi kudai kuwa ushairi wa wagunduzi si wa Kiswahili kwa sababu haufwati urari wa vina na mizani na hivo umbo lake ni tafauti na la mashairi ya Kiswahili. Fauka ya hayo, wachanganuzi wa mashairi ya Kiswahili wana maoni kwamba mashairi ya Kezilahabi ni aina mpya ya mashairi ya Kiswahili. Lengo la makala haya ni kugeuza mwendelezo wa fikira hii. Lengo hili limefikiwa kwa kutumiya uainishaji wa mashairi ya Kiswahili uliyotolewa na Mwanajadi Nabhany kwamba umbo la shairi linatokana na mpangiliyo maalumu wa sauti. Kwa kuchanganuwa umbo la shairi moja la Kezilahabi kupitiya kigezo cha bahari ya utumbuizo, ambayo Nabhany ameiorodhesha kuwa bahari mojawapo ya mashairi ya kijadi ya Kiswahili, tumeona kwamba ushairi wa Kezilahabi una sifa zote, ama karibu zote, za bahari hiyo. Kwa sababu hiyo, tunahitimisha kuwa ushairi wa Kezilahabi ni ushairi wa Wanajadi.

## Utangulizi:

Tangu kabla ya miaka ya sitini pamezuka ubishi katika mawanda ya taalimu ya mashairi ya Kiswahili na haswa kuhusiana na umbo la mashairi hayo (Abedi, 1954:2). Makundi mawili yamejitokeza kutokana na majiliyo ya aina ya mashairi ambayo, kimachoni, yanaonekana ni mashairi mageni wala hayana asili wala fasili katika fasihi ya Kiswahili. Ni mashairi yasiyotunga urari wa vina wala mizani. Kwa ufupi, mashairi haya vina vyake vinabadilikabadilika na idadi ya mapigo (mizani) katika uneni wake unabadilika vilevile. Watafiti (Mazrui & Shariff (1976); Mazrui (1992); Indede (2008); Masinde (2006; haina tarehe)) waliyoandika kuhusu 'mgogoro' huu wameyapa majina mikao hii: 'mahafidhina', 'wanajadi', 'wanamapokeo', na mkao wa 'wanamageuzi', 'wanamapinduzi', 'wanahuriya'. Ruo (1989) amewaita 'wachokozi', Chacha (1992) amewaita 'waasi' na Mulokozi 'wanausasa' (katika Aiello & Gaudioso, 2017). Na sisi tutawatambulisha kwa 'wagunduzi' kama tutakavoeleza baadaye katika makala haya. Chembelecho Abdilatif Abdalla katika utangulizi wake wa *'Sikate Tamaa*, mtunzi kujinasibisha na kundi lingine lisilokuwa la

Wanajadi alihitaji 'ujasiri'. Kwa hivyo, ni mikao yenye kani za kitaasubi kama anavoshikiliya Chiraghdin katika utangulizi wa *Malenga wa Mvita* (1971:13-14).

Makala haya yataonesha kwamba mashairi yanayoitwa 'mapya', kama wanavodai kina Kezilahabi na hata Njogu (1995), si mapya wala si mageni, bali ni utanzu mmoja wa ushairi wa Wanajadi. Makala haya yataangaziya kigezo ambacho Wanajadi, pengine kwa kughafilika, wamekiratibisha kigezo hicho kama utanzu mmoja wa ushairi wa Wanajadi lakini walipotathmini mashairi ya kina Kezilahabi hawakukitiliya maanani. Tutatumiya uainishaji aliyoupendekeza Ahmad Sheikh Nabhany (1985), anayesemekana kuwa mwanajadi mshupavu, na uainishaji huu kufuatwa baada yake na mwanafunzi wake Shariff (1988) na waandishi wa vitabu vya mafunzo ya fasihi ya Kiswahili Mazrui & Syambo (1992), Njogu & Chimerah (1999). Tutatafsili maelezo ya sifa kuu ya aina ya mashairi ya Kiswahili kulingana na Nabhany na halafu tuangaziye data kutoka mashairi ya Kezilahabi. Baada ya kufanya hivo tunaamini itadhihirika wazi kwamba 'mgogoro' unaosemekana haustahili kuwako kamwe. Makala haya yataziba pengo lililopo kuhusu sifa za mashairi yanayodaiwa ni mapya na sisi kusema kwamba *ni mashairi ya Kiswahili* bila ya kufananishwa na tanzu nyingine za fasihi simulizi au andishi au ya jamii za Kiafrika kijumla.

Makala haya yatayachambuwa mashairi ya Kezilahabi kulingana na mihimili ya uanishaji mashairi ya Wanajadi kama alivyofafanuwa Nabhany (1985) na Shariff (1988). Makala haya hayatoangaziya mashairi ya watunzi wengine kwa sababu tunaamini sampuli ya data kutoka kwa Kezilahabi inatosheleza kutowa mwangaza kuhusu lengo la makala haya. Makala haya piya hayatotowa maelezo kuhusu sababu za kuzuka au historiya ya aina ya mashairi ya Kiswahili au maudhui ya mashairi ya kina Kezilahabi. Ni maelezo ya kisinkroniya kuhusu aina ya shairi na namna matini inavyolandana na ufafanuzi wa kifani wa wanajadi. Katika makala haya tutatumiya neno 'shairi' kwa maana pana ya utungo wowote wenye mpangiliyo maalumu wa sauti na wala siyo kama alivobainisha Shariff (1988) kwamba ni aina ya bahari ya ushairi. Hali kadhalika, katika makala haya tutatumia majina ya wanajadi na wanamageuzi kwa maana kama alivotumiya Mazrui (1992). Mwisho, tutatumiya maneno 'fasihi ya Kiswahili' kwa maana finyu ya kiuanajadi ya kimaeneo na kiwakati.

Mapitiyo yetu ya kazi zilizoandikwa kuhusu arudhi ya mashairi ya Kiswahili inatuonesha kwamba kunao wataalamu wanaodai kwamba ushairi wa Kezilahabi na 'kundi lake' ni mgeni na ni maenreleo yaliyopatikana kwa kuona watu wengine ulimwenguni wanavoandika mashairi yao kwa ainati nyingi (Indede, 2008; Topan, 1974). Kuna wengine waliyotaja tu kwamba ushairi wa aina hii (wa Kezilahabi) una asili katika fasihi simulizi ya kiafrika kwa ujumla bila kuhusisha Wanajadi (Wamitila, 2008, Mulokozi katika Aiello & Gaudioso, 2017). Kuna na wengine wametaja tu kwamba ni aina ya utumbuizo katika mashairi ya Kiswahili lakini wakayapa mashairi ya Kezilahabi kwamba ni tapo jipya (Masinde, 2006; Njogu, 1995; Abdulaziz, 1979). Hata Chiraghdin, ambaye ni mwanajadi asili, katika utangulizi wake wa *Malenga wa Mrima* (1977:3) anasema kwamba mashairi [ya kina Kezilahabi] hayamo katika ushairi wa Kiswahili na piya hayafai kuitwa guni kwa sababu hayakupotoka kivina; bali Sengo asema ni mashairi kwa Kiswahili lakini si ya Kiswahili (Njogu & Chimerah (1999:118). Makala haya ni tafauti na misimamo waliyochukuwa waandishi hawa kwamba ni *kitengo kipya* kilichovyazwa na kina Kezilahabi au *hakimo* ndani ya mashairi ya Kiswahili (msisitizo ni wetu).

### Fasili ya umbo la shairi

Katika kamusi ya *The Routledge Dictionary of Literary Terms* (2006:92) munaelezwa kuwa umbo ni namna jambo linavoonekana, ni kile kiwiliwili cha kazi ya kifasihi; mwili wake ni vina, mizani, mitindo ya lugha, na sentensi zilizotumika kuwasilisha maudhui ya mtunzi. Kwa hivo, kutokana na mwono wa nje wa kazi ya kifasihi ilivofinyangwa nriyo tunapata kujuwa maana ya umbo na kuitafautisha na miunri inayoijenga kazi hiyo. Ijapokuwa kuna ubishani kuhusu mgao huu wa fani na maudhui, hata hivo, ni kusahilisha welewa wa dhana hizi za fani na maudhui na tunakubali kuwa dhana hizi zinachangiyana.

Kulingana na Wamitila (2008:226) anasema kwamba, 'shairi ni utungo wa sanaa ya lugha na mpangilio maalum wa mishororo au wa kisauti...'.

Katika mpangilio huu maalumu wa kisauti wenye kuonesha umbo la shairi ndimo kijelezi cha utanzu wa shairi unajulikana. Kulingana na Masinde (2006:22) umbo la shairi ni sura ya nje ya utungo na hujumuisha: beti, mishororo, mizani, vipande, vina, kibwagizo, na Senkoro (1988) akaongezeya wizani. Asili ya umbo hili la shairi la Kiswahili kulingana na wachanganuzi wa mashairi ya Kiswahili ni nyimbo za asili zilizokuwa zikiimbwa katika jamii. Baada ya muda umahiri wa Waswahili ukaongezeka na urari wa vina na mizani ukaanza kuonekana na upeo wa ufanifu wa ushairi wa Kiswahili ulifanana na ushairi wa mataifa mengine ya ulimwengu. Ubora huu ulidhihirika kwenye misemele na hata methali (Mazrui & Syambo, 1992; Chiraghdin katika *Malenga wa Mrima*). Isipokuwa, Masinde (2006:13) anasema kuwa maendeleo ya ushairi yametokana na dini ya Kiislamu na Senkoro (1988) naye anasema yametokana na mfumo wa kiuchumi wa kimwinyi. Maoni haya tunayakataa kwa sababu ya kunasibisha umbo la ushairi wa Kiswahili na kuchipuka kwake kutoka mahali kwingine. Hivo, kutokana na kauli ya Masinde, Waswahili hawana chao cha asili yao ila ni ukopaji, fikra anayoipinga Abedi (1954). Tena, si sawa kwamba mfumo wa kiuchumi wa Kimwinyi ndiwo ulozaa ujumi wa mashairi kwa sababu suala la ujumi halihitaji mfumo wa kiuchumi kujichipuza; ni utwezaji wa Wanavitu kuwa chochote huzuka kwa sababu ya mfumo wa kiuchumi (Said, 1997:143). Hivo basi, umbo la shairi la Kiswahili lina uasili wa Uswahilini na huhusisha kuwako vipambanuzi kama vina, mizani, mishororo, beti, kuwako au kutokuwako urari wa vina, mizani, vipande, na kibwagizo.

### Umbo la shairi kulingana na Wanajadi

Tukimwangaziya mwanajadi Shariff (1988:42-44) anatowa nguzo muhimu katika shairi la Wanajadi nazo ni: mshororo, mizani, kina, kiwango, bahari, na mkondo. Kutokana na nguzo hizi muhimu za shairi la Wanajadi, Nabhany (1985:13) na Shariff (1988:44) wamekuja kutowa aina (bahari) za mashairi ya Kiswahili nazo ni kama zifwatazo:

i. Wimbo
ii. Shairi
iii. Zivindo
iv. Utenzi au utendi
v. Utumbuizo
vi. Hamziya
vii. Dura mandhuma/Inkishafi
viii. Ukawafi
ix. Wajiwaji
x. Tiyani Fatiha
xi. Wawe
xii. Kimai
xiii. Sama/Mahadhi

Kulingana na wao wawili, orodha hii si kamili kuna mengi mengine (Nabhany, 1985:13; Shariff, 1988:44) ambayo bado yanahitaji utafiti kuzumbuliwa. Jambo hili la kwamba kuna mashairi mengi mengine katika fasihi ya Kiswahili ndilo lililomfanya Shariff kuikosowa kazi ya Amri Abedi (1954). Shariff (1988:38) anaoneleya Abedi alipoifanya kazi yake kuwa ndiyo mwongozo wa mashairi ya Kiswahili, basi aliyoyasema Abedi ni machache *sana* (msisitizo ni wetu) kuhusu arudhi ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Katika sehemu hii ya uainishaji wa mashairi ya Kiswahili, Shariff, Nabhany, Mazrui & Syambo, Njogu & Chimerah wote wanatowa fafanuzi za kila bahari tulizoorodhesha hapo juu.

Bahari (Shariff, 1988:44) au utanzu (Mazrui & Syambo, 1992:47) ya/wa utumbuizo katika orodha iliyopo hapo juu, ndiyo tutakayoi(u)tumiya katika kuegemeza ushahidi wetu kwamba mashairi ya Kezilahabi, na wanamageuzi kwa jumla, ni mashairi ya Kiswahili kinda kindaki. Katika ufafanuzi wa tafsili anaoutowa Shariff (1988:52-53), mwanafunzi wa Nabhany katika ushairi, kuhusu utumbuizo anasema hivi:

> Kuna tumbuizo za aina tatu; aina ya kwanza na inayotungiwa zaidi ni ya utungo ambao hauna hisabu maalumu ya mizani, lakini mwisho wa kila kifungu au mshororo humalizikia kwa kina. Utumbuizo wa aina hii huweza kuwa na kina kimoja au zaidi. Mtungaji-mtumbuizaji hutumiya vina zaidi ya kimoja ili kumfanya msikilizaji asichokeshwe na sauti moja tu ya milingano. Tungo za aina hii kama tungo nyingi za Kiswahili zilitungwa kwa madhumuni ya kutumbuiza (au kuziimba).... Mshororo wa utumbuizo wa aina hii unaweza kuwa na mizani chache na unaweza kuwa na mizani nyingi sana.... Si lazima utumbuizo

> wala utungo wowote wa Kiswahili uandikwe kwa sheria zetu za leo tunazozitumia kuandikia nyimbo, tenzi, mashairi na kadhalika. [Utumbuizo] wa aina ya tatu, vilevile, huwa na vina vya mwisho tu, lakini una viwango.

Mambo tunayoweza kuyavuwa katika dondoo la Shariff kuhusu sifa za kimsingi za utumbuizo ni kwamba:

1. Utumbuizo hauna idadi maalumu ya mizani katika mshororo; zinaweza kuwa chache au nyingi sana
2. Utumbuizo huwa na vina mwishoni mwa mshororo
3. Kina katika utumbuizo kinaweza kuwa kimoja au zaidi
4. Ndani ya utumbuizo kuna kiwango (kituwo) ambacho hakina mlingamano kama kina
5. Kina hubadilishwa ili msikilizaji asichoshwe na mlingano wa kina
6. Tunaweza kutunga utumbuizo na tungo nyingine bila kutumiya arudhi
7. Madhumuni haswa ya utumbuizo ni kutumbuiza/kuimbwa.

## Uchanganuzi wa data

Shariff (1988:53) anatowa mfano wa utumbuizo maarufu wa kale uitwao Bwana Wendee Yungwa unoonesha lalamiko la mwanamke aliyegunduwa mumewe ameowa mke wa pili. Kipande cha utumbuizo huwo wasema hivi:

> Bwana wendee Yungwa koleya mashungwa, mimi humngoja kuwambiya kongo
> Hungoja toka nisimeme hata k’anguka k’enda kwa majongo
> K’amngoja nili na furaha, hata moyo k’afanya kisongo
> K’angoja, k’ingiya k’amwambiya k’ongo
> K’ampokeya mvungu na ucha k’auweka kula penye chango
> K’apokeya kitoka na yembe k’azitiya t’ini ya nlango
> K’amvuwa shungurere lake k’aliweka mbee za nlango
> K’antukuwa k’anchiya choni k’amfucha vumbi na uwongo
> K’ampaka mafucha kwa mai, k’anyowa kula penye jongo
> K’anvuwa dhake dha k’ondeni, k’anvisha dhangu dha urembo...

Dondoo hili la utumbuizo lina sifa za matumizi ya mizani na vina katika mishororo yake wakati wa kutongolewa. Mshororo wa mwanzo una mizani 24, wa pili una mizani 20, mshororo wa tatu una mizani 20, na mshororo wa nne una mizani 12 na hali kadhalika katika utumbuizo huu idadi zinapishana. Kuna kina cha mwisho pekee nacho ni –ngo. Unavoonekana utumbuizo mzima una ubeti mmoja pekee.

Katika shairi la Kezilahabi liitwalo Kisu Mkononi (katika Abdulaziz, 1979:103-104) anasema hivi:

> Wakati miaka inaibwa mmoja mmoja,
> Kurudi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo
> Siwezi, kama gurudumu, nitajiviringisha.
> Mtelemko mkali huu.
> Lini na wapi mwisho sijui.
>
> Mbele chui mweusi, nyuma mwanga
> Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu ya dhambi.
> Kisu! Maisha kafiri haya
> Kama kutazama nyuma au mbele
> Ni kufa moyo mzima!
>
> Sasa kama simba-mtu shauri nimekata.
> Ya nyuma sana nisijali, ya mbele sana niyakabili.
> Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka
> Nikifuata kamba kama ng’ombe aliyefungwa,
> Kila mpigo wa moyo wangu
> Huu mpigo muziki wa maisha.

Shairi hili limefanana kiumbo na shairi la Wanajadi/kimapokeo; lina beti, mishororo, kina, na mizani. Beti zake ni tatu. Kuna ubeti wenye mishororo mitano na ubeti wa mwisho una mishororo misita. Kina na mizani ya ubeti wa kwanza ni:

________________16 ja

________________15 ndo

________________16 sha

________________10 u

________________10 i

Tutaona kwamba mshororo wa kwanza una mizani 16 na kina chake ni –ja. Piya tunaona kwamba mishororo mingine ina 'vipande' na mingine haina 'vipande'.

Tukirudiliya sifa za kimsingi tulizoziorodhesha kutokana na kijelezi cha Nabhany kupitiya Shariff, tunaona kwamba mashairi yote mawili, Yungwa na Kisu, yana sifa hizi: Kwanza, kuna mishororo. Pili, kuna kina kinachobadilikabadilika katika Kisu na hakibadiliki katika Yungwa (ijapokuwa huko mbele kinabadilika). Tatu, kuna matumizi ya mizani ambayo inatafautiana katika kila mshororo wa mashairi yote mawili. Nne, shairi la Kisu linaonekana kufuata sharuti ya kutochosha msikilizaji kwa sababu ya kutokuwa na kina kimoja. Tano, shairi la Kisu halikufuata arudhi iliyozoeleka ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Na sita, shairi la Kisu limeonesha kuwa na mizani chache katika mshororo yake jambo lililothubutu katika kijelezi cha utumbuizo hapo juu. Saba na mwisho, ni kwamba shairi la Kisu laweza kuimbika kwa sababu ni kazi ya manju kutiya sauti/lahani katika shairi kama alivonambiya Ustadh Ahmad Nassir kwamba nyingi ya nyimbo za nduguye mwimbaji mashuhuri wa taarab Pwani ya Kenya, Juma Bhalo, ni mashairi yake (mazungumzo naye Mambasa 5.1.2018)

## Matokeo

Kutokana na uchanganuzi huu, ni wazi kwamba japo mashairi Kisu na Yungwa yana mfanano na kutafautiana katika mambo fulani, lakini mashairi yote mawili yana sifa zilizotolewa na Nabhany na Shariff kuhusu utumbuizo, na kwa upana zaidi, mashairi ya Kiswahili. Kwetu sisi, shairi Kisu na mashairi ya mfano wake ni mashairi ya Kiswahili na yanaweza kuthibitishwa kwa kutumiya arudhi/vigezo va Wanajadi. Chembelecho Shariff (1988:44) anasema kwamba bahari za ushairi wa Kiswahili ni nyingi sana hazina idadi na ndani ya bahari moja muna mikondo isiyo idadi. Kwa hivo, kina Kezilahabi wamefutuwa (wamekashifu/wameweka wazi) utanzu ambao upo katika mashairi ya Kiswahili wala si kitu kipya wala kigeni. Badala ya kuwaita wanamageuzi au wanamapinduzi na mashairi yao kuitwa mapingiti basi twastahili tuwaite wagunduzi kwa sababu wamefichuwa kitu kilichokuwa kimefichika katika ushairi wa Kiswahili. Chembelecho Mulokozi (katika Aiello & Gaudioso, 2017) alipowazungumziya waandishi wa fasihi ya kiafrika kwamba "waliogunduliwa"; kwamba wapo lakini wamefichwa, na mashairi ya Kezilahabi yapo katika mashairi ya Wanajadi ila yalikuwa yamefichika.

## Hitimisho

Katika makala haya tumejaribu kutowa ushahidi wa kupatikana kwa mashairi ya wanamageuzi katika mashairi ya wanajadi. Tumetumiya majina ya Kezilahabi na Nabhany, katika anwani ya makala haya, kama wawakilishi na vielelezo va makundi mawili yaliyojitokeza kuhusu ushairi wa Kiswahili. Tumetumiya kigezo cha Wanajadi kilichoratibishwa na Nabhany kuhusu aina na umbo la mashairi ya Kiswahili kuchanganuliya ushairi wa Kezilahabi na kuangaliya ujumuishaji wake katika mashairi ya Wanajadi. Uchanganuzi wetu umetuonesha kuwa ushairi wa Kezilahabi umo katika uwa wa Kiswahili kwa kuthubutika kuwa unafanana na bahari ya utumbuizo. Hatimaye, mfanano huu unatufanya tuhitimishe kwamba ushairi wa Kezilahabi si mpya wala si mgeni wala si kitengo kando bali ni ushairi wa Kiswahili kinda kindaki. Je, Mazrui (1988: xiv) umekoma ubishi huu?

## MAREJELEO


Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka: 19th century popular poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Abedi, K. A. (1954). *Sheria za kutunga mashairi na diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Aiello, F. & Gaudioso, R. (wah.). (2017). *Ushairi na uhuru: Mkusanyo wa tungo za Abdilatif Abdalla na Euphrase Kezilahabi*. Napoli: Universita degli studi di Napoli.

Chacha, C. N. (1992). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla: Sauti ya utetezi*. Dar es Salaam: Dares Salaam University Press.

Childs, P. & Fowler, R. (2006). *The Routledge dictionary of literary terms*. London: Routledge.

Indede, F. N. (2008). Mabadiliko katika umbo la ushairi na athari zake katika ushairi wa Kiswahili katika *Swahili Forum*, *15*, 73-94.

Masinde, E. W. (2006). *AKS 402: Swahili poetry*. Nairobi: Kenyatta University Institute of Open Learning.

Masinde, E. W. (h.t). Language and Swahili free verse: Disparities, implications and the way forward pdf.

Mazrui, A. & Shariff, I. N. (1976). A note on Kiswahili poetry katika *Kiswahili 46* (1), 65-70.

Mazrui, A. (1988). *Chembe cha moyo*. Nairobi: Heinamann Kenya Limited.

Mazrui. A. & Syambo, B. K. (1992). *Uchambuzi wa fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mazrui, A. (1992). Conservationism and Liberalism in Swahili Poetry: The Linguistic Dimension katika *Research in African Literatures*, *23* (4), 67-76.

Mohamed, M. (1977). *Malenga wa Mrima*. Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, S. A. (1980). '*Sikate tamaa*. Nairobi: Longman Kenya.

Nabhany, A. S. (1985). *Umbuji wa Kiwandeo*. Nairobi: East African Publishing House.

Nassir, A. (1971). *Malenga wa Mvita: Diwani ya Ustadh Bhalo*. Nairobi: Oxford University Press.

Njogu, K. (1995). Poetic Serialization: Kiswahili Metapoetry on Prosodic Knots

*Research in African Literatures*, *26*(4), 138-150.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Ruo, R. K. (1989). *Nguzo za ushairi wa Kiswahili*. Nairobi: Macmillan Kenya Limited.

Said, E. W. (1997). *Covering Islam: How the media and the experts determine how we see the rest of the world*. New York: Vintage Books.

Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia na tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Shariff, I. N. (1988). *Tungo zetu: Msingi wa mashairi na tungo nyenginezo*. New Jersey: The Red Sea Press.

Shariff, I. N. (1991). Islam and secularity in Swahili literature: An overview. Katik a K. W. Harrow (mh. ) (1991) *Faces of Islam in African literature* (37-58). Portsmouth: Heinamann Educational Books.

Topan, F. (1974). Modern Swahili poetry. Katika *Bulletin of the School of Oriental and African Studies 37*(1), 175-187.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.